**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Kumi na Tano – Tarehe 22 Mei, 2026**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua Zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2026/2027.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2026/2027.

## III. MASWALI:

**Wizara ya Fedha na Mipango:**

172. MHESHIMIWA MAHMOUD SHINENI ALI (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Wakati Serikali inafikiria kukuza na kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea nchini kutoka 400,000 hadi 500,000 kwa mwaka 2026, bado kumekuwa na vikwazo na changamoto nyingi zinazowakwaza watalii wanaokuja kutembelea Zanzibar, hasa

wanapoingia nchini kutozwa Tozo ya Bima ya Afya (Inbond Travel Insurance), Tozo ya Bima ambayo imekuwa ikitozwa mpaka kwa baadhi ya wageni wenye asili ya Tanzania (Diaspora), wanapoitembelea Zanzibar.

(a) Kwa nini Serikali haioni haja ya kuiondoa Tozo hii ya Bima, ili kuweza kuvutia zaidi watalii kutembelea nchini.

(b) Kwa kuwa Tozo hii ya Bima ya Afya kwa watalii haifanyi kazi upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Tanzania bara) na baadhi ya watalii huanza kushukia Bara na kufikia Zanzibar, kwa nini Serikali haioni kwamba, Tozo hii inaharibu taswira njema ya watalii kuongezeka Zanzibar.

(c) Ni ipi kauli ya Serikali juu ya Raia wa Afrika Mashariki, ambao hulipishwa Tozo ya Bima hii ya Afya (Inbond travel Insurance) wanapoingia Zanzibar.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

17. MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (Jimbo la Ziwani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa usafiri wa pikipiki (bodaboda) umechukua nafasi kubwa katika visiwa vyetu. Na kwa kuwa tangu usafiri huu uanze kushamiri ajali zimeongezeka maradufu jambo linaloathiri vijana wetu siku hadi siku kwa kupoteza maisha yao au kupata ulemavu wa viungo unaowapelekea kupelekwa nje ya Zanzibar kupatiwa viungo bandia.

Je, lini Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kitaanzisha Kituo cha Uhandisi wa Viungo Bandia (Faculty of Biomedical Engineering) ili kupunguza tatizo hilo kwa waathirika hao.

## Wizara ya Afya:

108. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Eneo la bustani liliopo katika Hospitali ya Mnazimmoja linadaiwa kumilikiwa na Mamlaka ya Mji Mkogwe ambayo ndiyo iliyojenga na kuimarisha bustani hiyo. Hata hivyo, tokea asili wakati shauri la kujengwa lilipotolewa eneo hilo lilikuwa ni mali ya Hospitali ya Mnazimmoja.

(a) Je, ni kwa Mamlaka yepi Mamlaka ya Mji Mkongwe imehodhi

eneo hilo la Hospitali ya Mnazimmoja kwa kulifanya la kwake.

(b) Je, endapo Hospitali watahitaji kulitumia kwa mdhumuni mengine kwa maslahi ya umma watafanyaje wakati Mamlaka ya Mji Mkongwe wameshalihodhi eneo hilo.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo:</u>**

321. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Utoaji wa ushauri wa kitaalamu wa kilimo (agricultural extension services) ni miongoni mwa nyenzo muhimu zinazochangia kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima.

Je, Serikali imejipanga vipi katika kuimarisha utoaji wa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima hususan katika mabonde ya Tibirinzi na Kitubwini yaliyopo katika jimbo la Chake Chake.

**<u>Wizara ya Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:</u>**

322. MHESHIMIWA ABDULWAHAB SAID ABUBAKAR (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Teknolojia ya Habari na Ubunifu:

Katika kufikia malengo ya uchumi wa kijiditali Zanzibar inahitaji upatikanaji wa huduma ya intaneti mijini na vijijini.

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha wananchi wanapata intaneti ya uhakika, salama na yenye gharama nafuu.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza matumizi ya TEHAMA katika biashara ili kuchochea ukuaji wa uchumi wa kijiditali Zanzibar.

**<u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>**

19. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Katika juhudi za kutaka kuifungua Pemba, Serikali imeanzisha utaratibu wa kupeleka meli za mizigo moja kwa moja katika Bandari ya Mkoani Pemba.

(a) Je, ni meli ngapi za mizigo zimeweza kutia nanga katika bandari hiyo ya Mkoani hadi sasa.

(b) Je, kuna changamoto gani ambazo zimejitokeza katika kulitekeleza lengo hilo.

398. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo linafanya operesheni zake katika nchi mbalimbali. Hata hivyo, hakuna maelezo kama Zanzibar inahusika vipi katika faida na hasara za Shirika hilo.

(a) Je, ni upi uhusika wa Zanzibar katika umiliki wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

(b) Je, kama Zanzibar itakuwa haimo katika umiliki wa Shirika hilo, kuna mpango gani wa Zanzibar kuwa na Shirika lake la Ndege hasa kwa kuwa hivi sasa Zanzibar imekuwa ni fikio kubwa (destination) la watalii kutoka pembe zote za dunia.

(c) Kwa kuwa zamani Zanzibar ilikuwa na ndege yake ya kuwasafirisha viongozi, ndege ile imeishia wapi na kuna mpango gani wa kuwa na ndege yetu wenyewe ya kuwasafirisha viongozi wetu wakuu.

## IV. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>

### <u>Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:</u>

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa mwaka 2026/2027.

**Zanzibar,**
**22 Mei, 2026.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA**
**<u>WAWAKILISHI, ZANZIBAR</u>**